# Pambazuko

Toleo Namba 0045 Jumatatu Septemba 4-10, 2023



# Uhaba wa mafuta wataanda

- *Waagizaji wakubwa wanayo tele*

Uk. 5

# Samia ateua majaji 24

- *Apangua uteuzi wake wa juzi*

Uk. 9

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

# Tahariri

## Tujipange kujiunga Brics

TOLEO lililopita la gazeti hili la Pambazuko, lilibeba habari kubwa ya namna nchi wanachama wa Umoja wa Brics walivyokuwa wakiizungumzia Tanzania.

Kwamba viongozi hao walikuwa na shauku ya kuona Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi zitakazojiunga na umoja huo kwa siku za usoni.

Hatua hiyo, Pambazuko lilidokezwa kwamba ilitokana na namna Tanzania, kupitia kwa Rais Samia Suluhu Hassan inavyojipambanua katika kuimarisha uchumi na kuhakikisha maisha ya watu wake yanakuwa bora zaidi.

Aidha, ikabainika kuwa kuimarika kwa uchumi, uongozi bora, amani, kuzungukwa na nchi nane, kuwa pembeni mwa bahari, ni miongoni mwa sifa ambazo kundi la nchi zenye uchumi unaokua haraka (Brics) zinatamani Tanzania kuwa mwanachama wake mpya.

Kundi hilo lenye nchi tano hadi sasa, Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini (Brics), linaona pia uwepo wa bandari, mtandao mzuri wa barabara na malighafi nyingi, kuwa miongoni mwa vigezo vya kuijumuisha Tanzania kuwa mwanachama wake.

Pambazuko lilidokezwa kwamba Tanzania ni nchi iliyojadiliwa zaidi na viongozi wakuu na wataalamu wa uchumi wa nchi za Brics waliokutana kwa ajili ya mkutano wao wa 15 katika Jiji la Johannesburg, Afrika Kusini kuanzia Agosti 22-24, mwaka huu.

Brics, kundi la kiuchumi lililoanzishwa rasmi mwaka 2006, likijumuisha nchi zenye uchumi unaokua haraka, limekuwa likielezwa na wachumi kwamba baada ya miaka 30 ijayo, litaongoza kwa kuwa na uimara wa uchumi duniani.

Tayari Brics imeanza kuhofiwa na Marekani, Umoja wa Ulaya (EU), Benki ya Dunia, na Shirika la Fedha ya Kimataifa (IMF), makundi ambayo Brics inatamani "kuyafuta" kwa imani kwamba yapo kwa ajili ya kunyonya zaidi kuliko kusaidia nchi zenye uchumi wa kati na masikini.

Pambazuko tunapenda kuiasa serikali kwamba, hatua ya "wakubwa wa Brics" kuonesha nia ya kutamani kuwa na Tanzania miongoni mwa wanachama wake wapya, ni njia sahihi ya kutufanya tuongeze bidii katika utendaji wetu wa kazi na hasa za kuzalisha mali na kuziuza nje ya nchi.

Kujiunga na Brics ni fursa kubwa ambayo, endapo itakuwa hivyo, basi uhakika wa kuongezeka kwa mauzo ya nje utakuwa mkubwa zaidi.

Brics, kwa namna inavyokuja kuwa soko kubwa na kitovu cha kukua kwa uchumi, ndiyo maana hadi sasa zaidi ya nchi 43 zimeomba kujiunga nao, lakini Tanzania inaangaliwa kwa jicho la pekee.

Ni vyema wataalamu wetu wa uchumi na maeneo mengine, kuongeza nguvu ya kuchunguza faida zaidi za Brics na kushauri serikali namna nzuri ya kufaidi kuwa mwanachama.

Tunashauri kwamba jambo hili lisifanywe kuwa siasa, litazamwe kwa jicho la uchumi zaidi na neema zinazoweza kuvunwa kupitia Brics na tujiunge haraka fursa hiyo ikitokea.

# MAGWIJI WANAPOKUTANA...




***Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Maugo (kushoto), akibadilishana mawazo na aliyekuwa mhariri na gwiji wa habari wa magazeti ya Uhuru na Mzalendo, Joe Nakajumo. Wahariri hawa walikutana hivi karibuni Dar es Salaam wakati wa moja ya semina zinazoandaliwa na wakuu wa taasisi za serikali kuelezea mafanikio yao kwa umma (Picha na Khalfan Said).***

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## NUKUU



***Kawaida, mafanikio hayaji kama ajali, bali yanakuja kwa kazi ngumu, uvumilivu, kujituma, kujifunza, kujitoa na zaidi ya yote mapenzi makubwa kwa kile unachofanya au kujifunza kufanya – Nukuu ya Kiswahili ambayo aliyeanzisha hajatajwa popote.***

# Uelewa

## Anabaki na nini akipokwa ubalozi?

**Na Abbas MWALIMU**

SIKU ya kwanza ya Septemba, mwaka huu – 2023, itabaki kuwa kumbukumbu kwamba Rais Samia Suluhu Hassan alimvua hadhi ya ubalozi Dkt. Willibrod Slaa.

Dkt. Slaa aliteuliwa kuwa balozi Novemba 23, 2017 na aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mpaka kustaafu kwake ubalozi, Dkt. Slaa alikuwa akihudumu katika kituo cha Stockholm, Sweden.

Sehemu kubwa ya jamii inaamini kuwa mabalozi huendelea kuwa na kinga na upendeleo wa kibalozi hata baada ya kumaliza majukumu yao na kurejeshwa nyumbani.

Ukweli ni kwamba kinga na upendeleo wa kibalozi hutumika pale tu balozi anapokuwa kwenye kituo chake cha kazi.

Balozi anaporudi nchini Tanzania anakuwa hana kinga wala upendeleo wa kibalozi.

Aidha, balozi anapostaafu kuiwakilisha nchi kwa mujibu wa sheria na kurejea nyumbani, anakuwa hana hadhi wala kinga yoyote ya kibalozi.

Kikubwa anachobaki nacho mhusika, ni hadhi ya kuitwa balozi na siyo vinginevyo.

Hadhi ya ubalozi huweza kuvuliwa na rais wa nchi husika peke yake.

Mfano, kwa mujibu wa Ibara ya 36 – sehemu ndogo ya kwanza - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaweza kumvua hadhi balozi na pia kumrejeshea.

Lakini, ikumbukwe pia kuwa mabalozi huweza kuvuliwa hadhi zao hata wakiwa bado kwenye majukumu yao.

Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 32 ya Mkataba wa Vienna unaohusu Uhusiano wa Kidiplomasia wa mwaka 1961.

Ikumbukwe kuwa Balozi Costa Mahalu aliwahi kuvuliwa hadhi ya ubalozi na baadaye kurejeshewa hadhi hiyo na Rais John Magufuli.



*Dkt. Willibrod Slaa*

Vilevile, Alphayo Kidata aliwahi kuvuliwa hadhi ya ubalozi na Rais Magufuli.

Ikumbukwe kuwa mabalozi wanapoteuliwa hula kiapo cha utii kwa mkuu wa nchi.

Kadhalika, mabalozi hutakiwa kuishi kwa kuenenda na Sheria ya Maadili wa Viongozi wa Umma Namba 13 ya mwaka 1995 hata baada ya kumaliza majukumu yao ya kuitumikia nchi katika vituo walivyopangiwa.

Pia, mabalozi hutakiwa kuishi katika viapo vyao hata wanapokuwa wamestaafu kuitumikia nchi.

Hivyo, kuvuliwa hadhi ya ubalozi kwa Dkt. Wilbraod Slaa si jambo geni nchini.

Aidha, siyo kweli kuwa mabalozi huendelea kuwa na kinga na upendeleo wa kibalozi hata pale wanapomaliza majukumu yao na kurudishwa nchini au kustaafu.

Tanzania iliridhia mikataba ya Vienna inayohusu Uhusiano wa Kidiplomasia na Kikonseli ya mwaka 1961 na mwaka 1963 mutawalia kwa Sheria ya Bunge Namba 5 ya mwaka 1986.

Mikataba hiyo ya Vienna (wa mwaka 1961 na 1963) hutoa kinga na upendeleo wa kibalozi pindi tu mabalozi wanapokuwa wanaziwakilisha nchi zao nje ya nchi husika.

# Uhaba wa mafuta watanda nchini

**Na Mwandishi WETU**

UHABA wa mafuta umeendelea kudhihiri katika maeneo mengi ya Tanzania, hasa Kanda ya Ziwa Victoria, Pambazuko linaweza kueleza.

Baadhi ya vituo vya kuuza mafuta vya wilaya za Chato, Mbogwe na Bukombe, mkoani Geita, jana vilifungwa baada ya kukosekana bidhaa za kuuza; mafuta ya petroli, dizeli na taa, kwa wateja

Pambazuko lilizunguka vituo kadhaa, na vingi vilikuwa havina mafuta katika wilaya hizo, isipokuwa vituo vya Lake Oil pekee.

Katika vituo vya Lake Oil, gazeti la Pambazuko lililozunguka katika maeneo kadhaa ya wilaya hizo, lilishuhudia misururu wa magari; makubwa kwa madogo pamoja na pikipiki, ikisubiri kununua mafuta.

Waandishi wa gazeti hili walielekea Mji wa Ushirombo ambako walibaini kutokuwepo kwa mafuta na kuamua kuendesha gari hadi Runzewe – kilomita 45, ambako walikuta mafuta. Hata hivyo, kama ilivyokuwa katika maeneo mengine, nako kulikuwa na foleni kubwa ya wateja katika kituo kimoja.

Wateja walisikika wakilaumu wamiliki wa vituo “vidogo kwa kuficha mafuta” kwa madai kwamba walikuwa wakisubiri kutangazwa kwa bei mpya ya mafuta.

“Sisi tunajua, hawa wenye kuuza mafuta, tunajua wanaficha mafuta ili wasubiri bei kubwa itangazwe na Ewura ili wauze na kupata faida kubwa,” alisema mteja mmoja aliyejitambulisha kwa jina moja la Masele. Alikataa kutaja jina la pili baada ya kuambiwa anazungumza na mwandishi wa habari.

Kama ilivyokuwa kwa Masele, wateja wa maeneo mengine katika Mkoa wa Geita, waliozungumza na Pambazuko, wamekuwa na imani kwamba wafanyabiashara - kila inapofika mwanzo mwa mwezi, wamekuwa wakificha mafuta kusubiri bei mpya kutangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Tanzania (Ewura).



*Naibu Waziri Mkuu na Wizara ya Nishati - Dkt. Doto Biteko*

Mbali na Mkoa wa Geita na baadhi ya wilaya zake kukabiliwa na upungufu wa mafuta, maeneo mengine nchini yamekuwa yakielezwa kuwa na uhaba huo.

Maeneo kadhaa ya Mkoa wa Tanga, mwishoni mwa wiki yaliripotiwa kukabiliwa na uhaba wa nishati hiyo muhimu katika kukuza uchumi.

Pambazuko jana lilifanya uchunguzi wake katika maghala ya kuhifadhi nishati hiyo, Dar es Salaam na kubaini kwamba kampuni nyingi zinazoagiza mafuta, zina kiasi kikubwa cha mafuta.

Maghala ya mafuta ya kampuni za TotalEnergies, Puma, Lake Oil yamebanika kuwa na shehena kubwa ya mafuta na kwamba vituo vyao vya kuuza nishati hiyo havina uhaba unaoonekana kuwakabili wenzao.

Pambazuko limebaini kwamba wafanyabiashara wenye vituo vya kununua mafuta rejareja kutoka kampuni kubwa za kuagiza mafuta, vinakabiliwa na ukosefu wa mafuta kwa kuwa havina mikataba ya ununuzi.

Gazeti hili linaendelea kuchunguza ni namna gani vituo vya mafuta vinabaki kufanya biashara ya “umachinga?”

Habari

# Mbowe asaidia mamilioni kwa jamii

Na Mwandishi WETU

CHAMA cha siasa siyo lazima kishike dola na kuongoza serikali ndiyo kiweze kusaidia wananchi.

Kazi ya kusaidia jamii, haisubiri chama cha siasa kuingia madarakani ndiyo wananchi watambue kwamba kipo na kwamba kinafanya kazi.

Wataalamu wa sayansi ya siasa duniani kote, wanaeleza na kushauri chama bora cha siasa, lazima kionyeshe utayari wa kusaidia wenye uhitaji, siyo kwa kupiga kelele tu, bali hata kwa kutoa misaada pale kinapoweza.

Ni kutokana na falsafa hii, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimekuwa kikisaidia jamii pale kinapoona kinaweza kufanya hivyo.

Katika kushikilia falsafa hii ya wanazuoni, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, ametoa michango mbalimbali ya kifedha kusaidia jamii akiwa katika ziara ya chama hicho inayoendelea kwenye mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria kwa miezi miwili sasa.

Hivi karibuni akiwa wilayani Kishapu, mkoani Simiyu, Mbowe, aliguswa na matatizo ya Shule ya Msingi ya Msomagedi, iliyopo Kata ya Msomagedi, ambayo inahitaji matundu ya choo na nyumba ya mwalimu.

Kutokana na hali hiyo, Mbowe alitoa fedha taslimu, Sh. milioni moja (1,000,000/-), kwa ajili ya kuchangia utatuzi wa changamoto hizo.

Akiwa wilayani Karagwe, Mkoa wa Kagera, wiki chache zilizopita, Mbowe alishiriki ibada katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Kayanga, ambapo alichangia Sh. milioni 10 (10,000,000/-) kwa ajili ya ujenzi wa kanisa la usharika huo.

Vile ile alichanga Sh. milioni mbili na laki nane (2,800,000) kwa ajili ya kugharamia uandaaji wa sare za kwaya nne za usharika huo.

Akiwa wilayani Misenyi, Mkoa wa Kagera, Mbowe aliguswa na tatizo la mwananchi aliyebomolewa nyumba, Mzee Terestori Ludovick, mwenye miaka 101 (pichani juu).



*Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe akimkumbatia Mzee Terestori Ludovick kutoka wilayani Misenyi, Kagera, baada ya kuchangia ujenzi wa nyumba yake. (Picha na mpigapicha Maalum).*

Ilielezwa kuwa nyumba ya mzee huyo ilivunjwa na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi kwa maelezo kwamba ilijengwa kwenye eneo linalomilikiwa na mammala hiyo.

Mbali na mzee Ludovick, wananchi wengine wengi walihamishwa kwenye maeneo yao ya asili yaliyopo kwenye Mji wa Mutukula, wakidaiwa ni wavamizi na kwamba walichukua maeneo hayo kinyemela wakati wakitambua kwamba siyo mali yao halali.

Hata hivyo, yapo madai kwamba maeneo waliyokuwa wakiyakalia sasa yamekabidhiwa kwa mwekezaji kwa ajili ya shughuli za ufugaji.

Kutokana na sababu hizo, wananchi hao hawakuambulia hata senti ya fidia.

Kutokana na mzee huyo kukosa nyumba ya kuishi, Mbowe alichangia ujenzi wa nyumba yake. Alitoa Sh. milioni mbili (2,000,000/-).

Chadema kupitia kwa kiongozi wake mkuu, Mbowe, chama hicho cha upinzani kimekuwa kikitoa misaada ya kijamii kwa watu wenye uhitaji na hatua hiyo inachukuliwa kuwa ndiyo moja ya sababu nzuri za kuwepo kwa mfumo wa vyama vingi Tanzania.

# Hii Tume ya Mipango itatuvusha?

Na Mwandishi WETU

WAKATI Tanzania iko mbioni kuandaa Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo Kuelekea mwaka 2050, Rais Samia Suluhu Hassan ameteua wajumbe wanne wa Tume ya Mipango katika Ofisi ya Rais, kuanzia Agosti 30 mwaka huu - 2023.

Lengo kubwa la Rais Samia ni kuongeza kasi ya maandalizi haya. Swali kubwa kutoka kwa Watanzania ni je, hawa watatuvusha?

Wajumbe hao ni Omar Issa, Balozi Ombeni Sefue, Balozi Ami Mpungwe na Maryam Salim Ahmed Salim.

Omar Issa, amekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa Kitengo cha Rais cha "Matokeo Makubwa Sasa" (BRN) wakati wa Rais Jakaya Kikwete; na Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa Kituo cha Kuchochea Uwekezaji katika Afrika (ICF)

Balozi Ombeni Sefue, alikuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa zamani, Balozi Mstaafu na mwakilishi wa Tanzania wa Kudumu katika Umoja wa Mataifa, New York, Marekani.

Balozi Ami Mpungwe, Mkurugenzi wa zamani Katika Wizara ya Mambo ya Nje, aliyesimamia Masuala ya Ukanda wa Afrika na Mashariki ya Kati, Balozi wa zamani wa Tanzania nchini Afrika Kusini, Mwenyekiti na Mjumbe wa Bodi mbalimbali nchini.

Maryam Salim Ahmed Salim, ni Meneja Mkazi wa Benki ya Dunia huko Cambodia kwa sasa.

Majukumu ya Tume ya Mipango ni kubuni dira na miongozo ya uchumi wa taifa; kusanifu sera za kiuchumi, usimamizi wa uchumi, utafiti, na mikakati ya maendeleo ya taifa; na kufanya tathmini ya hali ya rasilimali za taifa kwa ajili ya kuendeleza na kuishauri serikali juu ya matumizi bora ya rasilimali hizo.


*Ami Mpungwe*


*Maryam Salim*


*Omar Issa*


*Ombeni Sefue*

Pia majukumu mengine ni kuchambua mwelekeo wa vigezo muhimu vya kiuchumi ikiwa ni pamoja na urari wa malipo, ujazo wa fedha na bei na kuishauri serikali ipasavyo; kuchambua sera zilizopo kwa nia ya kuimarisha utekelezaji wake na kupendekeza sera mpya pale inapoonekana ni muhimu.

Tume hiyo pia inaelekezwa kufuatilia utendaji wa kila siku wa sekta mbalimbali za uchumi na kuhakikisha kuwa hatua zinazofaa zinachukuliwa ili kutatua matatizo yoyote ya kiutendaji yanayoweza kugunduliwa katika sekta hizo.

Aidha, tume hiyo inawajibika kuhakikisha miongozo juu ya uhusiano wa kiuchumi na mataifa mengine na mashirika ya kimataifa imeandaliwa; kuandaa mikakati ya kitaifa ya idadi ya watu; na kutoa miongozo ya uundaji wa Mpango wa Taifa na kufuatilia mchakato wa maandalizi ya mipango ya muda mrefu, mipango ya muda wa kati na mipango ya muda mfupi.

Kadhalika, Tume ya Mipango inapaswa kusimamia utekelezaji wa uamuzi wa serikali kuhusu masuala ya mipango na usimamizi wa uchumi; na kuchambua masuala yoyote ya kijamii na kiuchumi na kupendekeza kwa serikali sera na hatua zinazofaa kuchukuliwa kwa maslahi ya taifa.

# Tangazo


Ukiwa Bukoba...
Furahia Nono Freshi Juisi
Pata juisi (sharubati) ya matunda halisi iliyoandaliwa kwa usafi wa hali ya juu kwa kujali afya ya mteja.
Kunywa juisi ya;
Embe
Passion
Parachichi
Karoti
Nanasi/pinacolada
Tende
Tikiti
Pia tunandaa juisi mchanganyiko maalum wa matunda ili kuondoa uchovu na magonjwa nyemelezi (detox) na pia smoothie.
Nono Freshi Juisi
Wasiliana nasi kwa namba hii:
*0753949488*

# Samia ateua majaji 24

Na Mwandishi WETU

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesikia kilio cha Mhimili wa Mahakama kwa kuteua majaji 24 ili kuongeza ufanisi na kasi ya kutoa haki nchini Tanzania.

Uteuzi wa majaji 24 aliufanya jana na taarifa hiyo kuifikia Pambazuko usiku wakati gazeti hili likienda mitamboni.

Taarifa ya Ikulu iliweleza kuwa miongoni mwa majaji hao, wanne wanakuwa majaji wa Mahakama ya Rufani na 20 ni majaji wa Mahakama Kuu.

Majaji wanne wa Mahakama ya Rufani ni Jaji Lameck Mlacha, Jaji Paul Ngwembe, Jaji Mustafa Ismail na Jaji Abdul-Hakim Issa.

Pamoja na majaji hawa wa Mahakama ya Rufani, Rais Samia pia amewapa ujaji mawakili wa kujitegemea, baadhi ya wasajili wa mahakama na karani wa Baraza la Mawaziri.

Sambamba na hatua hiyo, Rais Samia pia ameteua na kufanya mabadiliko kidogo katika uteuzi wake aliofanya hivyo karibuni.

Katika uteuzi wake wa wiki iliyopita -Agosti 30, alimteua Balozi Prof. Kennedy Gastorn kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na sasa anakuwa Naibu Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Orodha ya kamili ya majaji hao pamoja na uteuzi mwingine ni kama ifuatavyo;

**a) Uteuzi wa Katibu Mkuu**

Amemteua Balozi Stephen Patrick Mbundi kuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki atakayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki. Balozi Mbundi atachukua nafasi ya Balozi Prof. Kennedy Godfrey Gastorn ambaye ameteuliwa kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**b) Uteuzi wa Naibu Katibu Mkuu**

Amemteua Balozi Said Shaib Mussa – Balozi wa Tanzania, Kuwait kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Balozi Mussa anachukua nafasi ya Balozi Fatma Rajab ambaye ameteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania, Qatar.

**c) Uteuzi wa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Amemteua Balozi Prof. Kennedy Godfrey Gastorn kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Balozi Prof. Gastorn anachukua nafasi ya Dkt. Evaristo Longopa ambaye ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

**d) Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani**

i) Amemteua Mhe. Jaji Lameck Michael Mlacha kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani. Kabla ya uteuzi Jaji Mlacha alikuwa Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu, Kigoma.

ii) Amemteua Mhe. Jaji Paul Joel Ngwembe kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani. Kabla ya uteuzi Jaji Ngwembe alikuwa Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu, Morogoro.

*Inaaendelea Uk. 10*

Habari

# Samia ateua majaji 24

*Inatoka Uk. 9*

iii) Amemteua Jaji Mustafa Kambona Ismail kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani. Kabla ya uteuzi Jaji Ismail alikuwa Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu, Divisheni ya Rushwa na Uhujumu, Dar es Salaam.

iv) Amemteua Jaji Abdul-Hakim Ameir Issa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani. Kabla ya uteuzi Jaji Issa alikuwa Jaji wa Mahakama Kuu, Zanzibar.

**e) Uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu**

i) Amemteua Dkt. Evaristo Longopa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Dkt. Longopa alikuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

ii) Amemteua Bw. Wilbert Martin Chuma kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Chuma alikuwa Msajili Mkuu wa Mahakama ya Rufani Dar es Salaam.

iii) Amemteua Bi. Sharmillah Said Sarwat kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bi. Sarwat alikuwa Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam.

iv) Amemteua Bw. Arnold John Kirekiano kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Kirekiano alikuwa Naibu Msajili Mwandamizi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam.

v) Amemteua Bi. Martha Boniface Mpaze kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bi. Mpaze alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Jumuishi katika Masuala ya Mirathi na Familia, Dar es Salaam.

vi) Amemteua Bw. Ferdinand Hilali Kiwonde kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Kiwonde alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu.

vii) Amemteua Bw. Said Rashid Ding'ohi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Ding'ohi alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Iringa.

viii) Amemteua Dkt. Angelo Kataraiya Rumisha kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Dkt. Rumisha alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam.

ix) Amemteua Bi. Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam.

x) Amemteua Bw. Ntuli Lutengano Mwakahesya kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Mwakahesya alikuwa Naibu Karani wa Baraza la Mawaziri, Ofisi ya Rais Ikulu, Dodoma.

*Inaendelea Uk. 11*

# Samia ateua majaji 24

*Inatoka Uk. 10*

xi) Amemteua Bw. Griffin Venance Mwakapeje kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Mwakapeje alikuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Wizara ya Katiba na Sheria, Dodoma.

xii) Amemteua Dkt. Dafina Daniel Ndumbaro kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Dkt. Ndumbaro alikuwa Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dodoma.

xiii) Amemteua Bw. Emmanuel Ludovick Kawishe kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Kawishe alikuwa Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dodoma.

xiv) Amemteua Bw. Abdallah Halfan Gonzi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Gonzi alikuwa Mjumbe wa Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) na Mhadhiri Msaidizi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

xv) Amemteua Bw. Kamazima Kafanabo Idd kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Idd alikuwa Mhadhiri Msaidizi Chuo cha usimamizi wa Fedha (IFM), Dar es Salaam.

xvi) Amemteua Bw. Frank Muyoba Mirindo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Mirindo alikuwa Mhadhiri Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), Tanga.

xvii) Amemteua Bi Hadija Ally Kinyaka kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bi. Kinyaka alikuwa Wakili wa Kujitegemea Kampuni ya Uwakili ya Lawhill Co. & Advocates, Dar es Salaam.


xviii) Amemteua Bi. Aisha Ally Sinde kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bi. Sinde alikuwa Wakili wa Kujitegemea Kampuni ya Uwakili BOWMANS Tanzania, Dar es Salaam.

xix) Amemteua Bw. Hussein Salum Mtembwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Mtembwa alikuwa Wakili wa Kujitegemea na Mmiliki wa Kampuni ya Uwakili ya HM Noble Attorneys, Mtwara.

xx) Amemteua Bi. Irene Daniel Musokwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bi. Musokwa alikuwa Wakili wa Kujitegemea na Mshiriki katika Kampuni ya Uwakili ya FC Attorneys, Dar es Salaam.

Uteuzi huu ni kuanzia tarehe 03 Septemba, 2023.

# Tangazo


Bukoba Raha
... Bukoba kuna senene
... Bukoba kuna maji safi na salama
Lakini Bukoba kuna G-smart Sauna & Steam Bath (Bafu la kuoga kwa mvuke).
Ukiwa Bukoba ama unaishi, usisahau kupata huduma G-smart Sauna & Steam Bath.
Hakika hautajuta na ona fahari kusimulia wengine huduma za G-smart Sauna & Steam Bath. Faida za Sauna na Steam Bath ni nyingi, lakini chache ni zifuatazo:
- Inaboresha afya ya moyo na mishipa
- Huondoa uchovu wa mwili na misuli
- Kuondoa msongo wa mawazo (stress)
- Kuzuia magojwa ya kukakamaa kwa misuli
- Inaboresha na kuhuisha mfumo wa usingizi
- Kuondoa sumu na kufanya ngozi nyororo zaidi
Wasiliana na G-smart and Steam Bath walioko Barabara ya Kashozi na wapigie simu kwa namba: 0626 265725 / 0767 291 670

# Wakamata 'magaidi' Kampala

**Na Mwandishi MAALUM**

HALI ya usalama katika Mji Mkuu wa Uganda, Kampala, jana ilikuwa tete baada ya kuwepo kwa taarifa za kufanyika ugaidi.

Habari zilienea zaidi baada ya makachero wa Jeshi la Polisi nchini humo kuvamia moja ya kanisa na katika jiji hilo lenye pilikapilika nyingi na kumkamata mtu mmoja; mwanaume ambaye alikuwa na vilipuzi.

Taarifa ya chumba cha habari cha TRT zinaeleza kuwa Polisi wapipata fununu za kuwepo tukio la kigaidi na waliweka "mitego yao" ambayo ilimtia mikononi mwao kijana anayekadiriewa kuwa na umri wa miaka 28.

Inaelezwa kuwa kijana huyo alikamatwa na baadaye wenzake, wanaodaiwa kupanga njama hizohizo, nao walitiwa mbaroni.

Polisi wanadai kwamba walitumia mbinu za kikachero kuweza kuwakamata wahusika hao na kwamba sasa wanaendelea kuwahoji ili kubaini mtandao wao na kwanini mwamepanga kufanya mashambulizi hayo.

"Tulipata maelezo ya kijasusi mapema asubuhi kuwa kuna njama ya kushambulia maeneo ya maombi leo," amesema msemaji wa Polisi katika Jiji la Kampala, Patrick Onyango.

"Vilevile tulipata taarifa kuwa mmoja wa washukiwa hao alikuwa tayari ameshafika mjini. Kwa hiyo tulimfuatilia na tukamkamata na sasa anaendelea kutupa maelezo ya kina na lengo lao hasa limesikumwa na kitu gani," aliongezea Onyango.

Polisi wamesema kuwa mshukiwa huyo wa miaka 28, alikutwa na bomu lililokuwa ndani ya kidishi cha chakula na waliweza kulitawanya.

"Mshukiwa huyo alizuiliwa alipokuwa akikaribia kuingia katika Kanisa la Pentecostal, Lubaga Miracle Centre, katika kitongoji cha Lubaga kusini mwa Kampala," alisema Patrick Onyango.

Bado hakuna maelezo iwapo



*Rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museven*

mshukiwa huyo alikuwa akifanya kazi na kikundi chochote kinachojulikana, japo kumekuwa na mashambulio awali ambapo wanamgambo wa ADF, wenye uhusiano na kundi la kigaidi lijulikanalo kama Daesh, wamekuwa wakitajwa kuhusika.

Kwa mujibu wa Idara ya Upelelezi ya Uganda, mamlaka zilikuwa zikiwasaka watu wengine watatu wanaoaminika kuwa pamoja na watu hao wawili waliokamatwa jana asubuhi.

Inaelezwa kuwepo kwa kundi la vijana waliosambaa maeneo kadhaa nchini Uganda ambao wana njama za kutaka kufanya mashambulizi ya kigaidia.

Tayari Uganda imesema imejipanga kuhakikisha kwamba nchi inakuwa salama na kutoa tahadhari kwa yeyote atakayekuwa na nia ya kudfanya ugaidi atakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Hapo awali ADF lilikuwa kundi la waasi wa Uganda, lakini lilitimuliwa zaidi ya miongo miwili iliyopita na kukimbilia katika misitu ya mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambako limekuwa na makao yake.

Kundi hilo linaelezwa kujipanga upya kwa ajili ya kushambulia maeneo kadhaa ya sala; hasa makanisa katika miji mikubwa na sehemu za biashara, hasa maduka makubwa.

# Tangazo


100% TRUSTED BRAND
PROUDLY TANZANIAN PRODUCT
DOR EASY WASH
LIQUID SOAPS
USAFI WAKO
NI JUKUMU LETU
MANUFACTURED BY: DOR EASY WASH
P.O BOX 80159 KIBADA, KIGAMBONI | DAR ES SALAAM - TANZANIA
MOB: +255 715 771 123 | EMAIL: DOREASYWASH@GMAIL.COM

# PCTL yasaidia Zanaki kupata kompyuta

**Na Mwandishi WETU**

LENGO mojawapo la Rais Samia Suluhu Hassan, ni ujenzi wa Tanzania yenye serikali inayoendesha shughuli zake kidijitali; uchumi na jamii.

Sasa Shule ya Sekondari ya Zanaki, Dar es Salaam, imejiunga katika safari ya kutekeleza lengo hili baada ya kufadhiliwa vifaa vya tehama.

Wafadhili wameipatia shule hiyo vinu 30 vya kompyuta, kiibodi, monita 30, betri 30 za kutunza umeme wa dharura, printa moja, skana moja, projekta moja, na seva tatu.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa shuleni hapo kwa mkuu wa shule hiyo, Delvine Koka, Ijumaa iliyopita, Septemba Mosi, 2023, kwa ufadhili wa asasi ya Tehama kwa Wote ya Tanzania, ikishirikiana na asasi ya The Trade Desk ya Marekani.

Asasi ya Tehama kwa Wote inafadhiliwa na Kampuni ya Power Computers Tanzania Limited (PCTL).

Akizungumza wakati wa hafla ya kupokea vifaa hivyo, Mkuu wa Shule ya Zanaki, Delvine Koka, aliwashukuru wafadhili kwa hisani hiyo na kuahidi kuvitumia vizuri kwa manufaa ya shule.

"Vifaa hivi vitakuwa chachu kubwa katika kurahisisha ufundishaji wa somo la kompyuta na utekelezaji wa shughuli zingine zinazohitaji matumizi ya vifaa vya tehama. Tunasema asanteni sana kwa taasisi za The Trade Desk na Tehama kwa Wote kwa msaada huu mkubwa wa vifaa," alisema Koka.

Makabidhiano ya vifaa hivyo vya tehama yalishuhudiwa na Pilly Ngarambe, aliyekuwa mgeni rasmi, kwa niaba ya Ofisa Elimu wa Jiji la Dar es Salaam.

Ngarambe aliwapongeza wafadhili kwa juhudi zao za kuchangia kwa hiari kwenye utekelezaji wa mipango ya serikali ya awamu ya sita, chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Jambo hili ni kubwa kwa sababu linaunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza matumizi ya tehama katika shule zote," alisisitiza Ngarambe.

Katibu wa taasisi ya Tehama kwa Wote, Aveline Malamsha, alisema kwamba pamoja na utoaji wa vifaa hivyo, tayari wamefanya hivyo katika shule zingine tatu, na wataendelea kufanya hivyo katika shule nyingine za Tanzania.

Mtendaji Mkuu wa kampuni ya PCTL inayofadhili asasi ya Tehama kwa Wote, Shakil Dharamsi, akizungumza katika hafla hiyo aliongelea umuhimu wa tehama katika zama hizi.

"Katika zama hizi ukosefu wa weledi na ustadi wa kutumia teknolojia ya tehama ni changamoto inayopaswa kutunyima usingizi, maana changamoto hii inawanyima wengi ajira, na wale walio kwenye ajira hushindwa kuzalisha kwa tija kwa sababu ya uhaba wa ustadi wa teknolojia hii," alieleza Dharamsi.



*Mkuu wa Shule ya Sekondari Zanaki, Delvine Koka (mwenye hijab katikati) akiwa anapokea vifaa vya kompyuta kutoka kwa mfadhili wa Tehama Kwanza, Shakil Dharamsi (Picha na Mpigapicha Wetu).*

## Tangazo


Tangaza na
Pambazuko
EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi
Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.
Kwa bei nafuu sana
0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

# Damu ya Mwangosi kutegua unafiki

Na Simon MKINA

NIMELIA. Nikalia na kulia tena na tena, kila napoona picha ama kusikia wengine wakimlilia mwandishi mwenzetu.

Nalia zaidi nikiona waandishi waliokuwa karibu zaidi na Daudi Mwangosi, yule mwandishi wa Kituo cha Televisheni cha Channel 10, aliyekuwa akiripoti kutoka Iringa.

Napata uchungu zaidi napolazimishwa kutazama damu, matumbo, moyo, maini na mapafu ya Mwangosi, binadamu aliyezaliwa, akalelewa, akasoma, akaanza kazi zake, akaoa, akapata watoto wanne kupitia tumbo la mkewe, Itika.

Mimi siyo daktari, sikuwa na lazima kuyaona maungo ya ndani ya Mwangosi, lakini nimelazimishwa na watu, binadamu kama yeye. Hawa ni hayawani wasiokuwa na chembe ya utu.

Hata daktari, mwenyewe hana ulazima wa kuona matumbo ya mtu, hadi kuwepo sababu maalum ya upasuaji.

Nina hakika hata askari wa Polisi hawakufundishwa kuua waandishi, lakini sijui nini kimewakumba. Sasa wameamua kuanza kuua waandishi. Wameua mjumbe.

Hakika kifo cha Mwangosi, kama ilivyo kwa binadamu awaye yote, kinaleta simanzi. Kinasikitisha na zaidi sana kinapotokea kwa kulazimishwa. Tena hiki chake, kimelazimishwa na walinzi wa amani, wenye jukumu la kulinda uhai wake, sasa wao wamekuwa chanzo cha kuuondoa kwa nguvu za ziada na haraka mno.

Matumaini yangu ni kwamba, pamoja na kumlilia Mwangosi, huenda kifo chake kikaanzisha chachu ya kuwepo kwa umoja zaidi kwa waandishi, kazi zao kuthaminiwa zaidi na kuheshimika.

Kifo hiki kinaweza kuwa njia ya kujitambua kwa waandishi huku kikijenga wigo utakaowapa nafasi ya kuthaminiana zaidi na kuvunja misambaratiko na minyukano isiyokuwa na tija kwao.



*Daudi Mwangosi*

Waandishi tumeshuhudia wakinyanyaswa, tena na wenzao; baadhi ya wakubwa katika vyumba vya habari wakishindwa hata kupigania maslahi ya waandishi wanaowajazia habari kwenye vyombo vyao.

Tumeshuhudia waandishi wa mikoani (nje ya Dar es Salaam) wakifiwa na wazazi wao, watoto wao hata wake zao, na vyumba vyao vya habari vikishindwa kuwasaidia hata vipande vya sabuni kusafisha mikono ya wachimba 'vyumba vya milele'.

Mbaya zaidi Tanzania imeshuhudia vyombo vya habari vikiwakana waandishi wao, hasa –correspondents, wale wa mikoani wanapopatwa na madhila, licha ya kuwafanyia kazi kwa muda mrefu, bila hata kuwaajiri rasmi.

Wanawakana, mara nyingi wanapopata matatizo, ingawa, nina uhakika ikiwa waandishi hao hao wanaowakana, kama wakishinda tuzo za kimataifa za tasnia ya habari, watasimama hata juu ya mapaa wakipaza sauti za kumpongeza na kujipiga kifua kwamba huyo ni mwandishi wao.

Tuvunje makundi ya ubaguzi ya wahariri kuthamini zaidi wahariri.

Ulale salama Mwangosi.

***Septemba 2, alitimiza miaka 11 akiwa kaburini. Makala haya yaliandikwa miaka 11 iliyopita wakati wa kifo cha Mwangosi. Hapa ni marejeo***

## Mapitio

# Hotuba iliyoliza watu wa Gabon

SIKU ya kufunga kampeni za uchaguzi mkuu wa Gabon uliofanyika Agosti 26, mwaka huu – 2023, mgombea urais kwa tiketi ya muungano wa vyama vitano, Albert Ondo Ossa, alihitimisha hotuba yake ambayo imeelezwa kuwa bora zaidi kutolewa na mwanasiasa.

Akifunga kampeni zake, kiongozi huyo aliyekuwa akipewa nafasi kubwa zaidi ya kuibuka mshindi, Ossa alieleza mambo mengi, lakini kubwa alionekana "kulilia ustawi na neema" kwa kila mwananchi wa Gabon.

Kiogozi huyo, akizungumza kwa uchungu, alisema;

"Wananchi wote wa nchi hii. Amkeni kutoka katika lindi la usingizi mzito ambao kimfanano haupishani sana na kifo. Tazameni idadi ya maskini vijijini. Hurumieni vijana wanaovuja jasho bila ajira mijini. Jiji la Libreville limejaza omba omba.

Kuwa na idadi kubwa ya makabwela juu ya ardhi ambayo imebarikiwa utajiri wa mafuta, ni laana.

Ni aibu kwamba wakati watu hapa wanakufa kwa njaa na kuzidiwa na ufukara wa kutosha, familia ya Ali Bongo na watu wake wanaishi maisha ya kitajiri kufuru na anasa.

Enyi watu wa mfumo na watiifu wa kulazimishwa wa Ali Bongo, safari hii imbeni na mhakikishe mnaogopa nguvu ya Mungu. Imbeni kwamba mmechoka kulinda dhambi ya wizi wa kura kwa mtutu wa bunduki."

Enyi watu mfumo, angalieni kipindi cha uchaguzi mnavyopiga, kutesa, na hata kuua wafuasi wa upinzani. Chaguzi za Gabon ni zaidi ya kuitazama filamu ya kutisha iliyoshutiwa kuzimu. Chaguzi za Gabon zinanuka jasho la mauti.

Enyi watu wa mfumo, enyi waheshimiwa, msikubali kutumiwa. Angalieni makazi yenu yalivyochoka kama mabanda ya njiwa.



*Albert Ondo Ossa*

Nani anayewatuma? Yaani mnaamua kusaliti nchi ya mababu na mabibi kwa kuwa tu mnafaidika kwa peremende za Ali Bongo? Yaani muende mafunzoni na kisha mrudi kuilinda dhuluma?! Kama ni familia ya Ali Bongo na vibaraka wake iambieni, "sasa yatosha."

Ardhi ya Gabon inalia, inasononeka, inaomboleza, inaugua. Kwa kuwa nyie mmekuwa sehemu ya watu mnaolinda wasaliti na wezi wa maliasili za taifa hili.

Simameni kuhakikisha haki inatangazwa pale inaposhinda.

Kama Gabon itaendeshwa kwa haki usawa na hofu ya Mungu. Kila mtu wa taifa hili atajihisi yupo paradiso."

Hii ni sehemu ya hotuba ya kiongozi huyo wa chama cha upinzani ambaye inaaminika aliibuka mshindi katika uchaguzi uliofanyika hivi karibuni, lakini "akapigwa chini" na mfumo na matumizi ya majeshi na tume ya uchaguzi.

# Riadha

## Mkenya 'kutifua vumbi' Marekani

**Na Mwandishi MAALUM**




BINGWA wa zamani wa New York City Marathon, Geoffrey Kamworor wa Kenya, atatumia mbio za Great North Run mjini Newcastle, Uingereza kujiandaa kwa New City Marathon itakayofanyika Novemba 5 huko Marekani.

Kamworor, ambaye alishinda New York City Marathon mwaka 2017 na 2019, atakutana na mshindi mara sita wa Great North Run Mo Farah mjini Newcastle hapo Septemba 10.

Mjini Newcastle pia kutakuwa na Muethiopia, Muktar Edris, na Wahispania wawili; Hamid Ben Daoud na Daniel Mateo, miongoni mwa wengine.

Bingwa mara tatu wa Nusu-Marathon Duniani, Kamworor amethibitishwa pia kushiriki New York City Marathon ambapo atakabiliana na bingwa mtetezi Evans Chebet.

Pia atakutana na wengine Waethiopia wawili' Mosinet Geremew na Shura Kitata, Mholanzi Abdi Nageeye, Mwisraeli Maru Teferi, Mbelgiji Koen Naert na Cam Levins kutoka Canada.

Orodha ya kinadada nyota wanaoshiriki New York City Marathon ni mshikilizi wa rekodi ya dunia mbio za kilomita 42 za wanawake Brigid Kosgei na mabingwa wa zamani Peres Jepchirchir (2021) na Edna Kiplagat (2010). Pia, kuna Mary Ngugi-Cooper na Waethiopia Letesenbet Gidey, Gotytom Gebreslase na Yalemzerf Yehualaw na Mwisraeli Lonah Salpeter.

• ***Taifa Leo***

# MKUBWA ZAIDI DUNIANI...



***Uyoga unaoaminika kuwa mkubwa zaidi duniani, umepatikana huko nje kidogo ya Jiji la Lusaka, Zambia. Haikujulikana mara moja uzito wake na endapo uyoga huo ni salama kwa matumizi ya binadamu ama vinginevyo. (Picha kutoka mitandao ya kijamii).***

TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION